TANGAZO LA SERIKALI NA. 147 la tarehe 8/3/2024

SHERIA YA UTOAJI WA LESENI ZA BIASHARA,
(SHERIA NA. 25 YA MWAKA 1972)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 29(1))*

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA UTOAJI WA LESENI ZA BIASHARA ZA MWAKA 2024

Jina

T.S NA. 626 la 2023

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Utoaji wa Leseni za Biashara za Mwaka 2024 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Utoaji wa Leseni za Biashara za Mwaka 2023 ambazo katika Kanuni hizi zitarejewa kama "Kanuni kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 3

2. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 3(1) kwa kufuta maneno "na yataambatishwa na taarifa nyingine muhimu ambazo mamlaka ya utoaji wa Leseni itahitaji".

Marekebisho ya kanuni ya 6

3. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 6(1) kwa kufuta maneno "inaweza kutoa kwa mtu huyo nakala ya leseni baada ya kupokea ada" na badala yake kuweka neno "itatoa kwa mtu huyo nakala ya leseni ndani ya siku tatu baada ya kupokea ada".

Marekebisho ya kanuni ya 11

4. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 11 kwa-

(a) kufuta maneno "uzembe au" yanayoonekana katika kanuni ndogo ya (2);
(b) kwa kuongeza baada ya kanuni ndogo ya (2) kanuni ndogo ifuatayo:

"(3) Kwa madhumuni ya kanuni hii "makosa ya

*Tangazo La Serikali Na. 147 (Linaendelea)*

mwombaji" maana yake ni-

(a) kujaza aina ya biashara ambayo siyo sahihi:
(b) kujaza jina la mmiliki wa biashara ambalo siyo sahihi; au
(c) kukosea kujaza sehemu ya kufanyia biashara.

Marekebisho ya kanuni ya 13

5. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 13(2) kwa kufuta neno "itafanyika" na badala yake kuweka neno "itawasilishwa".

Kufutwa kwa kanuni ya 16

6. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta kanuni ya 16.

Dodoma,
16 February, 2024

ASHATU K. KIJAJI
*Waziri wa Viwanda na Biashara*